# *Nabii Mwenye Haya*

Sasa Bwana na aongeze baraka Zake kwenye somo la *Nabii Mwenye Haya*.

2 Asubuhi ya leo tulishughulika sana na nabii aliyevaa joho la kuachiwa. Na tunajua usiku wa leo, kwa kuwa katika Maandiko, asubuhi ya leo, ya kwamba sisi wenyewe tunavaa joho la kuachiwa. Sisi. . . joho. Nami nina furaha sana kwamba ni joho la kuachiwa, kwa maana vazi hili tunalolivaa sasa limehesabiwa kwa Mungu kuwa haki, kupitia kwa Kristo Yesu. Wala hatuchukui vazi lililoliwa na nondo la theolojia ya mtu fulani ambaye ameliwa na nondo na nyenje, na kadhalika, akisema kwamba, "Siku za miujiza zimepita, na hakuna kitu kama u—uwepo wa kila mahali wa Roho Mtakatifu sasa." Lakini tumevaa joho la haki Yake.

3 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Si kwa uwezo wetu wenyewe, bali katika u—uwezo wa Bwana wetu Yesu.

4 Na nitakaposhuka Yordani, ninataka kuvaa joho Lake, nikilitumainia Lake. Nacho kile kivuli kikubwa cha lango lililowekwa mbele yetu sote, kinachoitwa "mauti," kila wakati moyo wetu unapopiga, tunasogea mdundo mmoja karibu na pengo hilo kubwa ambalo kila mwanamume na mwanamke hana budi kupitia. Na nitakapolifikia pengo hilo, pamoja na nyinyi waaminio, nina furaha sana kujua kwamba siendi huko nikiwa na hili moyoni na akilini mwangu, kwamba nimefanya jambo kubwa. Ninaenda huko, nikikiri na nikijua kwamba mimi ni mwenye dhambi, na nikijua hili, ya kwamba, nataka kujivika majoho ya haki Yake; pamoja na ushuhuda huu, kwamba, "Ninamjua katika nguvu za kufufuka Kwake." Kwamba, atakapoita kutoka kwa wafu, nataka kutoka.

5 Sasa, mandhari na mchezo wetu wa kuigiza umewekwa usiku wa leo kwa ajili ya somo letu, wa siku nyingine katika Israeli, ambayo ilikuwa karibu miaka mia kadhaa baada ya wa—wakati wa Eliya. Mengi mema na mabaya yalikuwa yamekuja katika utawala wa Israeli. Na sasa tuko kwenye hiyo mandhari usiku wa leo. . .

6 Asubuhi ya leo tulikuwa kwenye mandhari ambapo palikuwa na uigaji mwingi wa kimwili, jinsi ambavyo shule ya manabii walikuwa huko juu wakijifunza kuwa manabii. Na jinsi walivyokuwa rahisi, hata wasingeweza kuelewa nguvu za Mungu. Walifikiri kwamba zile nguvu zilikuwa zimemwinua Eliya na kumtupa huko nje mlimani mahali fulani, nao wakatuma kikosi cha usakaji wamtafute. Wakati, Elisha alijua, vizuri kabisa, ya kwamba Mungu alikuwa amempeleka Utukufuni. Kwa maana, hakuwako. Mungu

alikuwa amemchukua, naye akaepuka mauti kwa kwenda Nyumbani kwa Mungu, juu ya gari la Moto na farasi wa Moto. Kisha tunaona ya kwamba seminari zao na kazi zao za theolojia yao wenyewe haikufanya kazi. Ilihitaji kuteuliwa pamoja na wito wa Mungu kufanya nabii wa Mungu.

7 Na sasa, usiku wa leo, tunaona Israeli katika hali ya kurudi nyuma. Israeli ilikuwa na mambo yake mema na mabaya. Ilikuwa ni mfano kamili wa kanisa siku hizi. Wakati mwingine walikuwa kwenye upeo, huo wakati mwingine wakawa chini bondeni. Hilo ndilo linalohitajika kutufanya tuthamini jambo jema. Hilo ndilo wanaloliita kanuni ya kutofautisha.

8 Mtu mweusi wa Afrika kamwe hakujua ya kwamba yeye ni mweusi, ngozi yake, mpaka alipomwona David Livingston. Naye akasema . . . Ndipo akagundua ngozi yake ilikuwa nyeusi, kwa sababu ya Livingston ilikuwa nyeupe. Ni kutofautiana.

9 Usingejua jinsi ya kuuthamini mchana kama hukuwa na usiku. Usingejua jinsi ya kuthamini mwanga wa jua kama hukuwa na siku yenye mawingu. Kamwe hungejua jinsi ya kuthamini haki, isipokuwa ulikuwa na udhalimu. Kamwe hungejua jinsi ya kuthamini afya njema, isipokuwa umekuwa na afya mbaya, afya mbaya. Ni wale tu . . .

10 Na hiyo ndiyo sababu ninafikiri ya kwamba tutaithamini Mbingu sana, kwa sababu tumeishi duniani wakati mmoja. Nami nadhani kanuni ya kutofautiana . . . Sababu ya sisi kumthamini Roho Mtakatifu sana, usiku wa leo, ni kwa sababu tuliishi kwa muda mrefu sana katika kanisa ambalo lilitwambia kwamba hakuna kitu kama hicho. Sababu ya sisi kumthamini, usiku wa leo, ni kwa sababu tumekuwa na upande ule mwingine. Na hivyo ndivyo Mungu amekusudia iwe, kwa sababu watu Wake wamekuwa na mema na mabaya yao. Huwezi kujua jinsi ya kuthamini kilele cha mlima, isipokuwa umekuwa bondeni. Na, kwa hivyo, kamwe hujui jinsi ya kuyathamini maji mazuri isipokuwa umekunywa mabaya siku moja. Na kisha wewe—wewe . . . Kotekote, ni kanuni ya kutofautiana.

11 Sasa, Israeli walikuwa katika mojawapo ya hali zao za kurudi nyuma, na ni jambo la jinsi gani walilokuwa wamefanya!

12 Sasa, Israeli walikuwa watu waliochaguliwa, walioteuliwa, waliotengwa, ambapo Mungu alikuwa amewachagua Israeli kwa kusudi moja halisi, kwamba damu ya Israeli inapaswa kuwa mkondo wa damu safi kuliko zote, kwa maana kutoka katika ukoo huo angekuja Masihi Mwenyewe.

13 Kote kote katika Agano la Kale, Mungu alijitokeza katika mwanadamu. Mungu alionekana katika Ibrahimu, kama mwaminio wa imani. Mungu alionekana katika Daudi, kama mfalme. Alionekana katika Yusufu, kama haki. Alionekana katika Musa, kama nabii, kuhani, mtoa-sheria. Alionekana kote katika nyakati, katika nabii. Yeye daima alijitambulisha

Mwenyewe katika wanadamu, kwa sehemu, kwa njia ya nabii, mfalme, kuhani, mtoa sheria, kadhalika. Lakini, ndani ya Kristo, Yeye alikaa ndani Yake, utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili, na akijua kwamba Roho huyu hatimaye hana budi kupata mahali pa kupumzikia. Juu ya Eliya, alikuwa mtu wa haki ya Mungu. Alitangaza haki ya Mungu. Na, Musa, yeye alikuwa mtoa-sheria, kwamba ufuate nyayo ama uondoke. Katika mambo haya yote, Mungu aliwakilishwa. Lakini alipomjia Kristo, Yeye alikuwa mkamilifu, utimilifu wote wa Uungu kwa jinsi ya mwili ulikaa ndani ya Kristo.

14 Naye Mungu alijiwakilisha Mwenyewe mara moja katika utimilifu, hapo awali. Katika kitabu cha Mwanzo, kwa mfano wa Melkizedeki, "Ambaye hakuwa na baba, hakuwa na mama; hakuwa na mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa miaka yake, wala mwisho wa maisha yake." Naye alikuwa kuhani, Mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu, wa Mungu Aliye Juu Sana, Ambaye alikuwa hana mwanzo wala mwisho. Hakuwa mwingine ila mfano tangulizi wa Bwana Yesu Kristo. Maana, Yeye alikuwa Mfalme wa Salemu, ambaye ni Mfalme wa Amani, ambaye ni Mfalme wa Yerusalemu. Naye alikuwa mfano tangulizi. Hata mzee wetu Ibrahimu alimtolea zaka. Alikuwa mfano tangulizi wa kuja kwa Bwana Yesu. Melkizedeki yuyo huyo alikutana na Ibrahimu huko nje kwenye nyanda kabla ya kuangamizwa kwa Sodoma na Gomora. Ndipo—ndipo akakutana naye baada ya Sodoma na Gomora, wakati Ibrahimu alipomtolea fungu la kumi la nyara zote alizoteka kutoka kwa mfalme.

15 Mambo haya yote yamekuwa vivuli, yamefananishwa na Kristo. Na sasa, vivuli vyote vya watakatifu wa Agano la Kale, mema na mabaya yao, vilikuwa ni kivuli na mfano, na mifano kwetu leo.

16 Sasa, tunaona ya kwamba Israeli hawakupaswa kuchanganyisha ndoa. Ndoa zao zilipaswa kuwa kati ya wao kwa wao, sio Mwisraeli kufunga ndoa na Mmataifa kamwe, lakini walikuwa waudumishe safi mkondo wao wa damu. Na hata wa leo, ninaamini mkondo wa damu wa Kiyahudi ndio mkondo—mkondo wa damu ulio safi kuliko yote juu ya uso wa dunia leo, ni Myahudi. Bado wanamtazamia huyo Masihi. Lakini, Yeye. . .Tunajua kwamba amekwisha kuja; na macho yao yalipofushwa, ili tupate nafasi ya toba kupitia Kristo.

17 Sasa, wakati wa utawala wa Ezra, wana wa Israeli walikuwa wamerudi nyuma. Walikuwa wametoka na kuwachukua wanawake wa Moabu, nao walikuwa wamewachukua wanawake wa Waamori, na Waperizi, na wengi wa mataifa hayo mengine. Na hawakuwa wamewaoa tu, bali walikuwa wakifanya uasherati miongoni mwao, uchafu, na kuchafua mkondo wenyewe wa damu, ambao ni mkondo wa uhai.

18 Na hiyo ni picha ya jinsi gani leo ya makanisa yetu,

jinsi wanavyoanguka kutoka kwenye mstari wa kuchongea wa mtindo wa kale ambao Mungu aliweka kwa ajili ya kanisa. Maagizo ambayo tulipaswa kuishi kwayo, kanisa linafanya uasherati na ulimwengu. Limeenda nje ulimwenguni, na kuanza kuchezacheza ulimwenguni.

19 Sasa, jambo hili lilikuwa limemwaibisha nabii sana, hata, alipokuja mbele za Mungu, aliaibika usoni mwake. Mara ya kwanza aliposikia habari zake, kisha akaona u—upotovu wa maadili ya watu wake, ilimuumiza sana mpaka akaketi chini na kujipaka mafuta, akang'oa nywele na ndevu zake, naye alikuwa na moyo mzito mbele za Bwana, katika maombi. Ndipo wakati dhabihu ya jioni ilipotolewa, aliingia hekaluni na kupiga magoti na kuona haya mbele za Mungu, kwa ajili ya dhambi za watu.

20 Sasa, hakuona haya kwa ajili ya barabara nyekundu ya mtaa wa makahaba. Hakuona haya kwa ajili wanywaji pombe kwenye maficho ya kuzimu, ingawa ni mabaya yawezavyo kuwa. Lakini, aliona haya kwa sababu ya dhambi za wateule.

21 Na tunachohitaji leo ni manabii wengine zaidi walio na Mungu wa kutosha mioyoni mwao kuona haya Mbele za Mungu, kwa ajili ya dhambi za watu wanaojiita watu wa Mungu na kufanya jinsi wanavyofanya. Tumeleta aibu ya jinsi gani mahali hapa! Maadili ya watu wetu. . .

22 Hili si somo rahisi kuzungumzia. Ninaweza kuwazia mambo mengi ambayo yalikuwa rahisi kuzungumzia. Lakini, ndugu, kama mtu fulani hatajitokeza katika siku hii ya dhambi, ya uzinzi tunayoishi, na kuukemea, itakuwaje? Mtu fulani hana budi kuzungumzia jambo hilo. Mtu fulani hana budi kuliweka mbele za watu.

Labda Ezra hakutaka kufanya hivyo, lakini ilikuwa moyoni mwake.

23 Basi unapomwona mtumishi wa Mungu akiwa mwaminifu sana mpaka amelala kifudifudi huku mikono yake ikiwa hewani, akimwomba Mungu, na kuona haya kwa sababu ya uovu wa watu, ndipo utaona uamsho ukianza. Mtu hawezi kukaa Uweponi mwa Mungu, kanisa haliwezi kukaa Uweponi mwa Mungu, chini ya toba, isipokuwa Roho Mtakatifu ashuke na kutoa upako na nguvu kuanzisha huduma ya Mungu mle ndani miongoni mwa watu hao. Haina budi kuwa!

24 Nionyeshe mtu. Nionyeshe Calvin mwingine, Knox, Finney, Sankey, ama yeyote wa wale wanaohisi mzigo wa watu, atakayelala kifudifudi na kulia na kuomba mbele za Mungu. Tutumie John Smith wa kanisa la Baptisti tena, ambaye aliomba usiku kucha kwa ajili ya maovu ya watu, mpaka macho yake yangevimba yafungike kesho yake asubuhi, kutokana na kulia, mpaka mke wake angemwongoza mezani na kumlisha kifungua kinywa chake kwa kijiko. Nionyeshe John Wesley tena, kijinga

cha moto kilichonyakuliwa kutoka motoni, nitakuonyesha uamsho.

25 Wanachofanya siku hizi, tunawapigapiga mgongoni. Tunauita *hivi* na *vile*, na uamsho, wakati hakuna uamsho kwake. Hiyo ni kweli. Kuna kuchochewa kwa mhemko wa kidini miongoni mwa watu, lakini hakuna uamsho.

26 Walikuwa na kundi la kidini siku hizo. Walikuwa na misisimko siku hizo, lakini walihitaji uamsho.

27 Mbona, ndugu na dada yangu mpendwa, maadili ya taifa hili yamekuwa duni sana hata yangemfanya mbwa aone aibu. Yangemfanya mbwa aone haya kama angeweza kufanya hivyo, utovu wa uadilifu wa watu wetu! Watu, hata miaka mingi iliyopita, mambo tuliyo nayo, ta—taifa limefanya, mambo ambayo watu wamefanya! Yote ni ukosefu wa maombi.

28 Kanisa ambalo lilikuwa, halikuamini katika sinema, hawangewaruhusu watoto wao kwenda kuona sinema. Wangesusia sinema. Na, siku hizi, mbona hata wananinii... Walikuwa na sinema nyumbani mwao wenyewe. Kila nyumba ina televisheni.

29 Katika mahali ambapo walikuwa wakifikiri ni vibaya kunywa pombe, mahali ambapo walikuwa wakifikiri...John Barleycorn, jinsi alivyokuwa mkaidi. Siku hizi, asilimia sitini za wanaojiita Wakristo hunywa pombe ya kijamii angalau mara moja kwa mwaka. Kisha wanafanya shamshamra, kwenye Krismasi, wakati wanapokuwa na sherehe yao. Kwa sababu, wamechukua elimu kupachukua mahali pa wokovu. Kamwe haitafaulu.

30 Tunachohitaji ni uamsho. Tunajifungia plasta za sugu, tunazitoa; plasta nyingine ya sugu, tunaitoa, na bado tunaona uchungu upo. Tunachohitaji siku hizi sio mabadiliko ya kijamii, sio mazungumzo ya kiakili. Tunachohitaji siku hizi ni utiaji wa Damu wa mtindo wa kale uliotumwa na Mungu kutoka Mbinguni. Plasta za sugu hazitafaa kitu. Tuna anemia. Tunahitaji nyongeza ya Damu. Tunahitaji kurudi kwenye Injili ya mtindo wa kale unaohitaji toba mbele za Mungu. Na si maungamo ya macho makavu ya kupeana mikono; bali uamsho wa Roho Mtakatifu uliotumwa na Mungu pamoja na kumiliki utakaso wa Damu ya Bwana Yesu Kristo ndani ya kila moyo wa mtu. Tunahitaji uamsho uanze Kanisani, na kuenea kote nchini. Tutakufa, tutaangamia, tumetoweka, bila uamsho wa aina hiyo.

31 Nimechefukwa na kuchoshwa sana kuona maskini uamsho duni wa Hollywood, unavyoitwa, ambapo watu wanaingia na kuchochewa kimhemuko kwa saa kadhaa, na, au siku moja au mbili, au juma moja au mawili, na kuondoka wala hakuna lingine. Ndugu, unaweza kuwa katika ninii...kuchochewa na uamsho. Unaweza kuwa na mhemuko. Unaweza kuwa na nia

njema. Mambo hayo yote ni sawa, lakini hatuhitaji hayo siku hizi.

32 Tunahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu, kubadilisha mhemuko, na akili, na mtazamo, tabia, maisha ya watu, na kuwarudisha kwenye njia sahihi tena. Nje ya kuwekewa Damu kutoka Kalvari, marekebisho yetu yote hayatafaa kitu.

33 Hatuhitaji U.N. Tuna U.N. huko, nao wangefanya nini? Jina la Mungu kamwe haliitwi. Wanaogopa kuliita. Iliuliziwa wakati mmoja, na kikundi cha makasisi, "Kwa nini hawakufanya maombi?" Wakasema, "Inaweza kumwudhi mtu mwingine, mmoja wa hao wengine ambao hawakumwamini Mungu."

34 Loo, tunachohitaji ni uamsho. Haijalishi kamwe inamwudhi nani, tunapaswa kuihubiri Injili na kukemea kabisa. Kweli. Nisingekupa hata hela kwa mpango wowote ambao ulimwacha Mungu nje, iwe ni U.N., ama yale makubwa manne, chochote kile.

35 Mpaka taifa hili litakapotambua, kwamba tunakufa bila Damu ya Bwana Yesu Kristo; mpaka watu binafsi watakapotambua sa—sababu, kwamba tunakufa! Sababu ya sisi kufa, ni ukosefu wa dawa asili, njia, tiba, ambayo Mungu alitupa pale Kalvari.

36 Si ajabu inamfanya mtu aone haya! Si ajabu! Mhubiri halisi wa kweli hutazama kusanyiko lake na kujaribu kuwaongoza mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Na kuwatembelea nyumbani mwao, na kuwakuta wakivuta sigara, wakitoa mizaha michafu, kujiburudisha kwenye uwanja wa nyuma, na karamu za bia; wakitembea huku na huku mitaani, wasichana wao, na wanawake wa makamo, na kadhalika, na hata bibi aliyevaa kaptura ndogo. Mama huko nje mitaani na mtoto mchanga kwenye mkono mmoja, wamevaa kizinifu vya kutosha kuvutia usikivu wa muuzaji yeyote wa pombe aliyetembea mtaani; huku wakijiita Wakristo. Ingemfanya mtu yeyote wa kweli wa Mungu kuona haya, kumleta mtu kama huyo mbele za Mungu. Kweli!

37 Na kujiunga kote kwetu na kanisa na kupata tabaka bora, kumekuwa ni upuuzi, na kulikuwa hivyo siku hizo na kutakuwa hivyo siku hizi pia. Uturudishe kwa Mungu, si kwa kupenyeza elimu, si kwa kupenyeza matengenezo ya kidini, si katika kupenyezwa kwa aina fulani ya theolojia ya kujibunia. Lakini ubatizo wa mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu ulioshushwa kutoka kwa Mungu, kutoka Mbinguni, katika ujuzi wa kipentekoste wa kuyateketeza mambo ya kimwili. Na kurudisha mle kile kito ambacho Mungu alikusudia kiwe mle ndani, cha mwana na binti wa Mungu. Mpaka tutakapofanya hivyo, ndugu na dada, bado tutakuwa na nywele zilizokatwa, vipodozi, juu ya wanawake wanaovutia kizinifu; na wanaume wakinywa pombe, wakivuta sigara, na kujiita Wakristo; kwa sababu hawajui bora zaidi. Moyoni mwao, shina lenyewe la

kimwili linakaa mle, basi tunahitaji kusafishwa kwa kanisa, kutoka orofa ya chini hadi mimbarani. Amina. Na hiyo ni kweli.

38 Tunachohitaji siku hizi ni manabii wengine wanaoona haya. Mungu. . . Wakati mwingine watu wanapokuja kwenye mstari wa maombi, kuombewa, inaonekana kana kwamba wanaenda kwenye nyumba yenye sifa mbaya. Hiyo ni kweli. Wakija kumwomba Mungu jambo fulani, huku wakionekana kama Yezebeli. Tunachohitaji siku hizi ni kusafishwa kwa nyumba na kupasha joto moyo, kwa manabii wa Mungu ambao watasimama mimbarani na kutaja jambo hilo, na kusema yaliyo kweli na yasiyo kweli; na kuhubiri Injili bila kupatana, mpaka wenye dhambi waanguke sakafuni, na kulia mpaka Mungu amtume Roho Mtakatifu kuyasafisha maisha yao. Amina. Tunajua hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

39 Nilihubiri hapa si muda mrefu uliopita na kusema kwamba kila mwanamke katika mji huu alikuwa na hatia, kwa njia moja au nyingine, ya uzinzi. Wanayo. Wanawake hushuka katikati ya mji hapa na ni vigumu kununua nguo, isipokuwa iwe ile ambayo ni kama walimwagiwa ndani yake. Sipo hapa kuninii. . . Hili ni kanisa langu mwenyewe. Nina haki ya kuhubiri kile ambacho Roho Mtakatifu ananiambia nihubiri. Kweli.

40 Ngoja niwaambie. Sikukosoi, dada yangu. Lakini hivi Roho Mtakatifu hakufundishi tofauti? Kama hakufundishi, ninahofia hukumpata Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Roho Mtakatifu sio "kupaza sauti." Roho Mtakatifu sio "kucheza katika Roho." Roho Mtakatifu sio "kunena kwa lugha." Roho Mtakatifu ni haki. Mungu, tupe uamsho wa Roho Mtakatifu wa haki iliyotumwa na Mungu.

41 Hivi hutambui kwamba unapovalia hivyo na kutembea mtaani, nao wanaume wanakutazama kwa njia mbaya, kwamba kwenye Hukumu. . . Unaweza kuwa safi kama yungiyungi, mbele ya mumeo. Lakini, kwenye Hukumu, utakuwa na hatia ya kufanya uzinzi na mtu ambaye umejianika kwake.

42 Si ajabu itamfanya mtu aone haya! Si ajabu! Inafanya nini kwa Mungu? Wakati, Biblia ilisema, hapo mwanzo, ya kwamba, "Ilimhuzunisha, kwamba alimwumba mwanadamu." Iliuhuzunisha moyo wa Mungu, alipowatazama katika siku zile kabla ya maangamizi ya ile gharika, kwamba alimwumba mtu. Ilikuwaje? "Wana wa Mungu waliona binti za wanadamu kuwa ni wazuri." Ilikuwa ni upotovu. Ilikuwa ni upotovu wa kujuana kimwili. Jambo hilo ndilo lililowafukuza watoto wa Mungu kutoka bustani ya Edeni. Ni jambo hilo ndilo lililoileta hukumu ya Mungu, kuleta amani juu ya nchi. Jambo hilo ndilo lililowafanya waangamizwe. Ilikuwa ni mchanganyiko uo huo, kati ya wanawake na wanaume, uliosababisha Sodoma na Gomora kuzama chini ya Bahari ya Chumvi.

43 Ilisemwa na manabii. Ilisemwa na Bwana Yesu, kwamba, "Kama ilivyokuwa katika siku hizo, ndivyo itakavyokuwa kabla ya Kuja kwa Mwana wa Mungu." Tunaangalia siku hizi, na kuona ya kwamba kanisa linachukua mtindo wake si kutoka kwa Biblia, kutoka kwa Ruthu na kutoka kwa Naomi, na kutoka kwa Sara na wale walio katika Biblia. Lakini wanachukua mtindo, hata wanawake wa kanisani, wa Hollywood na mivuto yenyewe ya ibilisi.

44 Na jinsi ambavyo watu wetu, wanaojiita Wakristo, wanavyotoka huku na kupata njia za mtu huyu mwovu. Santuri hizi za Elvis Presley, vyovyote anavyoitwa, mmoja wa watu waliodanganyika sana, waliopagawa na ibilisi ambao nimewahi kusikia maishani mwangu. Arthur Godfrey na watu kama hao, na kusikiliza upuuzi wa aina hiyo kwenye redio zenu; na kukataa kusikia mahubiri ya Injili yakihubiriwa katika Biblia. Mungu awarehemu. Je, tuna roho ya aina gani miongoni mwetu? Hiyo ni kweli.

45 Si ajabu nabii wa Mungu aliona haya mbele za—za Bwana. Alijua huo ulikuwa ni udhalimu. Naye akasimama na kuitetea kesi, na kumwambia Mungu, "Sisi ni wadhalimu."

46 Nasi ndivyo tulivyo, marafiki, mpaka tunapoweza kurudia mahali hapa pa kuwekewa damu. Acheni kujaribu kujibandika plasta. Acheni kujaribu kuweka dawa. Uponyaji hauwezi kuja isipokuwa mkondo wa damu uwe sawa.

47 Hiyo ndiyo sababu watu wana kisukari. Kama mtu angejikata, labda hautapona. Kwa nini? Kwa sababu chembechembe nyekundu halisi za damu zimeliwa.

48 Nalo kanisa zima limeshikwa na kisukari. Na kila kidonda kinachotokea, badala ya kuendelea mbele, unakidonoa. Hakiwezi kupona. Ubinafsi, ulafi, utovu wa uadilifu, kila kitu kingine kilicho katika kalenda ya Mungu "kufanya makosa," kanisa linaokota tabia hizo. Wanaume wanakunywa pombe, wakivuta sigara, wakifanya mizaha michafu. Wanawake wakikata nywele zao, wakijipodoa, wakifanya mambo ya kila namna, wakivalia kizinifu wapate kukabiliana na watu. Mambo hayo yote ni kwa sababu ni ukosefu wa Damu ya Bwana Yesu Kristo kutusafisha na uovu wote. Amina. Hilo linaweza kuonekana kuwa gumu. Hakika, ni gumu, lakini ni Kweli.

49 Tusipozitangaza hukumu za Mwenyezi Mungu, utanaswa moja ya siku hizi katika mlipuko wa atomiki hapa, ambao utapeleka kila nafsi katika Umilele, kukutana na Mungu ambaye atatambua tu Damu ya Mwanawe, Kristo Yesu. Ushauri wangu: kukuona ukija chini ya Damu, ushauri wangu kwako ni kuwa sawa na Mungu, ushauri wangu kwako.

50 Vema, kwa nini hatuwezi kuwa na imani? Kwa nini tusiweze kuwa na uponyaji mkuu kuliko tulio nao? Kwa nini hatuwezi kujijenga vizuri kabisa? Ni kwa sababu tunajibandika plasta

za sugu; kwa sababu tunaweka vibandiko; tunaweka vipande vya tepu. Tunajaribu kuficha kitu hicho, badala ya kusema tunahitaji kuwekewa damu. Hatuna Damu. Hatuna Kristo. Usikubali kupumbazwa.

51 Usimruhusu ibilisi akupigepige begani, akisema, "Vema, mimi huenda kanisani."

52 Ibilisi huenda, pia. Hiyo ni kweli. Hakika alienda; alikuja kwa Mungu, akahudhuria kanisa huko Mbinguni; akaja mbele ya Kiti cha Enzi cha Mungu, pamoja na wana wa Mungu, akaketi pamoja nao; akaongea na Mungu. Akasema, "Umekuwa wapi?"

53 Kasema, "Kutembea huku na huku, kuzunguka-zunguka, duniani." Huko ndiko alikokuwa.

54 Kwa hiyo, ibilisi huenda kanisani. Ibilisi ni wa kanisa. Ibilisi hutenda kama Mkristo. Yeye ni mdanganyifu. Na kama hangetenda kama Mkristo na kufanya kama kanisa, asingekuwa mdanganyifu; hakuna mtu angeweza kudanganyika. Jambo pekee, ni tofauti kama nyeusi na nyeupe. Ni kinyume moja kwa nyingine. Lakini Yeye. . .Biblia ilisema, "Ingefanana sana hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini," roho hiyo katika siku ya mwisho. Enyi Marafiki, tuko hapo.

55 Ni wakati wa manabii wa Mungu, loo, ndugu, kwa wahubiri, kama ungelisema, kote nchini, kuanguka kifudifudi.

56 Mbona, hata hivyo, kuna makanisa milioni kumi na tisa ya Kibaptisti. . .Wabaptisti milioni kumi na tisa, hasa, Marekani; Wamethodisti milioni kumi na tatu; Walutheri milioni kumi na moja; Presbiteri milioni kumi. Rehema, wazia hilo! Na sikuzote wako kwenye mchezo wa mpira, kwa burudani. Na Jumatano usiku, na wakati mwingine Jumapili usiku, wanakaa nyumbani kusikiliza televisheni na redio, ya utani mfupi na mizaha wanayopata kutoka Hollywood. Nafsi yako inabingirika kwenye upuuzi wa aina hiyo.

57 Wakati, unapaswa kuwa na Biblia yako mahali fulani, umekaa mbele za Mungu, magotini mwako, ukiomba kwa ajili ya dhambi za nchi.

58 Nami nina hatia pamoja nanyi. Nimeamua. Kwa msaada na neema ya Mungu, ikiwa Mungu wetu atanipa nguvu za kufanya hivyo, nimeazimia kusonga mbele kuelekea kwenye mede ya wito mkuu katika Kristo Yesu, hata kifo kitakaponiweka huru. Mungu na awe msaidizi wangu kufanya hivyo! "Nisaidie," ndilo ombi langu. Kuyaona hayo matendo, na kuyaona niliyoyaona nanyi mmeyaona, na kubaki nyuma, na kuwa na anemia ya kiroho.

59 Nayo maskani hii inayojulikana katika ulimwengu mzima, maskini mahali hapa padogo pa saruji palipo pembeni, Mungu amewainua mbele ya taifa. Kweli.

60 Ninawazia yale Daudi, usiku mmoja, aliposema, "Mimi hapa, ninakaa katika nyumba ya mwerezi, na sanduku la Mungu wangu linakaa ndani ya hema." Akasema, "Nitamjengea nyumba."

61 Nathani, nabii, akasema, "Fanya yote yaliyo moyoni mwako, kwa maana Mungu yu pamoja nawe."

62 Usiku huo, Mungu akamtokea Nathani na kusema, "Da-. . .Nenda ukamwambie Daudi, 'Wewe ulikuwa nani, Daudi? Ulikuwa. . .Nilikutwaa katika zizi la kondoo, katika kuwaandama kondoo. Nami nikakufanyia jina kuu, kama la wakuu wa nchi.'"

63 Ni nani aliyekuwa katika maskani hii ndogo iliyoko hapa? Maskini kitu chenye mkondo wa maji, kilichotupwa nje kilicho pembeni mwa Barabara ya Nane na Penn, hata Jeffersonville haikujua ilikuwa wapi, na watu wanaokuja hapa. Na siku hizi, Mungu, kwa rehema Zake, amewainua na kuwafanya watu wakuu. Bombay, India inajua mahali maskani hii ilipo. Durban iliwajua; haya mataifa mengine yote. Afrika inajua mahali hapa palipo; India, Ujerumani, Uingereza, Ufini, Uswidi, Ulaya, Asia, hao wote, huko chini kabisa katika visiwa vya Thailandi, na huko chini, wanajua yote juu yake. Naye Mungu ametufanya kuwa mfano kwa watu. Na kuwazia, basi, baada ya Mungu kufanya hivyo, na sisi tunageuka na kusitasita katika mambo ya ulimwengu, na kuwa anemia ya kiroho yenyewe. Mbona, tunapaswa kuwa mnara wa taa ambao umewekwa juu ya kilima, mshumaa ambao hauwezi kufichika. Ee Mungu! Nina hatia kama ninyi wengine.

64 Ninachomaanisha, nataka—nataka toba ya mtindo wa kale, iliyotumwa na Mungu, na mwito wa kumrudia Mungu, hata wanaume na wanawake wanapoingia kwenye mlango ule, kwa mikongojo, watatoka bila hiyo. Vipofu watakapoingizwa mlangoni, watatoka wakiona. Viziwi wakija viziwi, watatoka wakisikia. Wenye dhambi wakiingia, weusi na waliochafuka kwa dhambi, watatoka, wameoshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo. Hivi hatuwezi kulifanya? Mungu aliwaita Israeli na kuwafanya kielelezo. Mungu alituita na akatufanya mfano, lakini tumemkosea Mungu, na inatutia aibu Mbele za Mungu.

65 Kuwazia hayo, mambo ambayo ametufanyia! Jinsi alivyotuinua kutoka kwenye zizi la kondoo! Jinsi ambavyo ametufanya kujulikana, kote duniani! Jinsi ambavyo ametufanyia jambo kuu! Na, hata hivyo, tunasitasita, na kuchanganyikana na kutoka nje, wala hatuonekani kuwa waaminifu. Hatufanyi maombi tena, na mambo, inaonekana, hayaendi sawa. Nasi tunajaribu kujibandikia mipango midogo, plasta za sugu, kupunguza maumivu. Huwezi kutuliza maumivu mpaka upate Damu nzuri, iliyo safi humo ndani ili kuponya kitu hicho. Kweli!

66 Wewe kata maskini sugu, nawe utajipatia kisukari, nacho kitaukata mguu wako. Usijaribu kutupilia mbali *hili,* na kukwepa *hili,* na kukata plasta ya sugu kwenye *hili.*

67 Lakini jambo la kufanya ni kuja moja kwa moja mbele za Mungu, na kusema, "Mungu, nina anemia, na ninahitaji Damu Yako ili inisafishe na dhambi yangu yote." Hayo ndiyo maombi yangu, naamini kwamba ni yako.

68 Yawazie mambo haya, rafiki. Moja ya siku hizi; inaweza kutukia upesi kabla ya mapambazuko asubuhi, kama inavyoweza kutukia miaka hamsini tangu leo. Bomu moja la roketi, moja ya hayo mabomu ya kobalti au haidrojeni lingeweza. . . Taifa zima liko katika tahadhari.

69 Uliliona kwenye gazeti hivi majuzi ambapo wanahitaji sayansi, Pentagoni, kujibia visahani virukavyo. Haikuwa ni hadithi ya kubuni. Haikuwa kitu kilichowaziwa. Ilikuwa ni halisi. Ilikuwa ni akili fulani. Waliruka kwa mpangilio wa vita. Wangeweza kusimama. Wangeweza kuanza. Wangeweza kusimama. Wangeweza kujua. Ilikuwa ni akili fulani. Wanajua hivyo. Watu walicheka. Walisema, "Ati visahani virukavyo?" wakalifanyia mzaha.

70 Lakini mnajua ninachofikiria? Yesu alisema, kabla hajaja, kutakuwako na ishara katika Mbingu juu. Je, mliona? Kabla hajaanza, kuiangamiza Sodoma na Gomora kwa sababu ya shughuli zao za kujuana kimwili, aliwatuma Malaika chini wakachunguze. Malaika wamekuja duniani katika miaka michache iliyopita. Wameonekana miongoni mwa watu; ninamaanisha, watu waaminifu waliooshwa kwa Damu wanaojua hivyo. Hata wamesimama na kupigwa picha zao. Hiyo ni kweli. Viumbe vya Kimalaika wamezuru, wakirudisha habari kwa Baba, kwamba dhambi imelundikana hata ni vigumu kwa nyota kung'aa. Mwezi. . . Dunia nzima inayumbayumba kama mlevi anayeingia usiku. Kweli.

71 Dhambi miongoni mwa Wakristo, miongoni mwa Wateule! Wameuza haki zao za mzaliwa wa kwanza kabisa, kwa ajili ya umaarufu. Mhudumu amebadilisha Injili kwa karamu ya kijamii. Ameibadilisha Injili ya mtindo wa kale iliyooshwa kwa Damu apate mambo ya kiakili pamoja na watu, kuhubiri kiakili, kuzungumza mambo ya jamii, na kuitumia Injili vibaya. Wengi wao wameingia hudumani, wakihubiri, na kutumia Injili kwa manufaa ya kibinafsi, kujipatia pesa. Wengi wao wana maghala makubwa na magari, na vitu ambavyo hawangeweza kupata kamwe, faida ya kibinafsi. Sio wote; ninashukuru kwamba bado kuna masalia.

72 Katika siku za Ezra, wakati Ezra alipoanza kulia, na kuita na kuikemea dhambi, mnajua kilichotukia? Wateule wote, waliomtumainia Mungu, walikusanyika karibu naye.

73 Tunachohitaji leo ni wanaume na wanawake. . .Wahubiri wenu wanahubiri, hayo makanisa, na kuita dhambi “dhambi,” na kuikemea, watu halisi wa Mungu wangekusanyika moja kwa moja kukuzunguka, na kukaa pamoja nawe. Hiyo ni kweli. Ni wakati wa kukemea, na kusema ipi ndiyo ipi, kutenganisha mema na mabaya. Mungu atujalie sisi, kwamba tutakuwa na ujasiri wa kufanya hivyo.

74 Wazia tu kile kingeweza kutokea. Na kama nilivyokuwa nikiwaambia, ninaamini, asubuhi ya leo, ama nilimsikia mtu fulani akisema, ya kwamba juu ya. . .Mmoja wa walinzi hawa wanaoshika doria; ninasahau mnavyowaita sasa, wakilinda bomu, au ndege zijazo. Si muda mrefu uliopita, kulikuwa na programu iliyokuja mahali fulani, ambayo walikuwa wameagiza makundi makubwa ya manowari, kukiweko na ndege mia tatu zenye mabomu ya atomiki na mabomu ya haidrojeni yakining’inia chini yake.

75 Si muda mrefu uliopita, kwenye uwanja mkubwa wa ndege huko Shreveport; mmoja wa hao wavulana aliongoka kule mikutanoni kwa Ndugu Jack. Alisema, “Tuna mabomu ya atomiki yanayoning’inia moja kwa moja kwenye mabanda yetu.”

Nikasema, “Hivi wewe. . .”

76 “Ndani ya. . .” Namaanisha, “Ndani ya—ndani ya ndege; nasi tungepanda juu na kufanya mazoezi nazo, kila siku.”

Nikasema, “Hivi huogopi?”

77 Kasema, “Hazijawekwa vyombo vya kufyatulia. Lakini tuko chonjo sana, hata katika muda wa dakika moja, sekunde sitini, tungeweza kuweka vyombo vya kufyatulia humo ndani na kuondoka. Na zimetiwa mafuta na ziko tayari, wangeweza kuruka hadi Uingereza nazo, mara moja.”

78 Mabanda makubwa yamewekwa baharini, kila mahali. Nao wanaiambia Urusi, “Thubutu kuangusha bomu moja! Rusha tu bomu moja la atomiki juu ya U.N. ama mahali fulani pale, muone kitakachotukia!”

79 Itakuwa nini? Urusi itavamiwa. Na kama wangefanya hivyo, na kuanza kuangusha hayo mabomu ya atomiki na haidrojeni, ingesababisha majibizano ambayo yangeiteketeza dunia iwe u—utambi, iyeyushwe kabisa. Unajua, haingepingana na Maandiko hata kidogo. “Kwa maana dunia itateketezwa, na mbingu pia.” Atomi za duniani zitaungua.

80 Tunaishi katika siku yenye hatari. Tunaishi katika siku ambayo watu wa ulimwenguni wanaogopa hata kufa. Watu mashuhuri, wana—wanahofu ni nani atakayelilipua hilo bomu la kwanza. Bomu la kwanza litakalolipuliwa, kitu hicho chote kitaingia kwenye m—mrushiano.

81 Unapaswa kuwa ndio wakati wa furaha sana ulimwenguni kwa Mkristo. Nyakati zitabadilika. Wazee watakuwa vijana.

Loo, jamani! Mauti yatatoweka upesi. Ugonjwa hautakuwako tena. Hakuna mikutano mingine ya maombi kwa wagonjwa. Hakuna tena mikutano ya maombi kwa waliopotea. Lakini Mungu atakuja na kuwachukua Wateule kutoka katika pepo nne za dunia, na kuwakusanya chini ya ubawa Wake mwenyewe, nasi tutaishi na kutawala pamoja Naye milele katika Mbingu Yake.

82 Loo, ndugu, dada, rafiki yangu, kama hujajiandaa usiku wa leo, naomba uwe tayari saa hii. Nakupa mwaliko uje kwa Kristo Yesu, usiku wa leo, na kupokea. Wewe ambaye umekuwa tofauti, wewe ambaye unajua kwamba hupo mahali ambapo unapaswa kuwa na Mungu, ninakualika madhabahuni pamoja nami. Ninamwalika kila mmoja wenu aje hapa, wala si kusema tu, bali kukaa hapa mpaka Mungu atakapoisafisha nafsi yako kutokana na kila kitu ambacho hakifanani na Yeye, mpaka unaweza kutoka hapa mtu mpya. Si ukiwa umevaa plasta ya sugu, bali kuondoka hapa pamoja na upaji wa Damu ambayo husafisha damu yako na hukupa Maisha mapya na tumaini jipya. Uondoke ukiwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Uondoke, sio ukipaza sauti, sio ukicheza dansi, sio sana sana . . . Mambo hayo ni sawa. Yote ni mali ya Kanisa. Yote ni ya Biblia. Lakini ninachozungumzia ni Roho Mtakatifu, upendo wa Mungu.

83 Kijana mwanamume mmoja alikuwa akizungumza nami hivi majuzi. Mama yake, mwanamke mpendwa. Nimemjua mwanamke huyo, nimekutana naye mara moja au mbili. Naye akasema, "Loo, mpenzi," kwa kijana wake, "njoo hapa, nataka uangalie. Nina mafuta mkononi mwangu." Naam, ninayo, pia. Ni mahali nimekuwa nikitokwa na jasho. Sasa, kasema, "Ninayo mafuta mkononi mwangu." Kasema, "Unaonaje kuhusu hilo?"

84 Ndipo mvulana huyo akamtazama mamaye, akasema, "Mama, nataka kukuuliza jambo fulani." Alitaka aombe, alimtaka aombe kwamba apate kutembea karibu zaidi na Mungu. Akasema, "Je, hayo mafuta yalipokuja mkononi mwako, yaliondoa hukumu yako yote? Je, yalikupa tukio la kupendeza pamoja na Mungu, wakati hayo mafuta . . . "

"La."

Kasema, "Basi ningeachana nayo." Ndivyo hivyo.

85 Loo, ulimwengu, ulimwengu wa kidini, watu wa kipentekoste, wanatafuta mazingaombwe. Ulimwengu, ulimwengu ulioelimika (unavyojiita), ulimwengu wa kimadhehebu, unatafuta suluhisho kuu ambapo wanaweza kuboresha dhehebu lao na kupata wafuasi wengi zaidi ndani yake, "milioni moja zaidi," mwajua.

86 Nayo ma—mataifa yanatafuta namna fulani ya kikosi cha polisi ambacho kinaweza kuleta ulimwengu mzima magotini mwao, na kuleta haki.

87 Ndugu, haiji kwa mazingaombwe ya upentekoste. Wala haiji kwa mashirika ya Kiprotestanti au na uongozi wa kikasisi wa

Katoliki. Wala haiji kwa pentagoni, au kufungua kurasa mpya. Inakuja kwa maisha yaliyojitolea kwa Yesu Kristo, kupitia kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kitu chochote pungufu ya hilo, ni makosa.

Na tuombe.

88 Nitamwomba dada yetu aje kwenye kinanda pale, piano, wakati huu. Tukiwa katika maombi, huku kila mtu ameinamisha kichwa chake, na kila mtu katika maombi. Nashangaa, kwa wakati huu, kama ungejaribu roho yako dhidi ya Neno la Mungu. Je, uko sahihi?

89 Baada ya ibada hii, kama nilivyowaambia. Nina mama mkwe amelala kule, mahututi. Sina budi kumwona. Yuafa. Marafiki wengine, ninaowajua hapa, ninaowatembelea, ambao ni mahututi, watu ambao wameketi katika kanisa hili. Loo, ndugu, dada, unashuka kule, pia. Huna budi kushuka huko.

90 Sasa, unasema, "Vema, na—najua hilo, Ndugu Branham. Ninakusudia kurekebisha jambo hilo, moja ya siku hizi." Lakini inaweza isiwe "moja ya siku hizi," kwako. Huenda ikawa hii ndiyo siku ya pekee.

91 Mtu huyo hakujua kabisa, akitoka California, akienda Michigan, hivi majuzi, akiwa na maskini mkewe hapa, akiendesha ga—gari; yeye katika pikapu, wakienda kwenye nyumba yao mpya. Alikuwa ndiyo kwanza amestaafu kutoka kwenye jeshi la Wanamaji. Alijua vema jinsi gani alipoanza safari asubuhi hiyo, labda kutoka kwenye bandari ya watalii, kwamba mke na mtoto wake mchanga wangekuwa maiti katika dakika chache? Lakini, juu tu ya Henryville pale, gari lao liligongana na basi. Naye dereva akafanya ni—ninii . . . gari lake karibu lipinduke kichwangomba, lakini lilimwua huyo mwanamke na msichana mdogo. Ninatumaini kwamba nafsi yao ilikuwa sawa na Mungu.

92 Majuma machache yaliyopita, wakati mimi na Ndugu Wood tulipopanda hapa ambapo ndege iliangukia nyuma ya mahali hapa, na kuwaangalia wakivuta vipande vya miili ya watu wanane, wakati vichwa na miguu na mikono vilikuwa vimetapakaa kila mahali. Wakiokota mwili, huku matumbo yakianguka kutoka mwilini mwa huyo mtu; mtu mzuri, labda, mtu maarufu kutoka Chicago. Wakati mtu huyo alipoingia kwenye hiyo ndege asubuhi hiyo, nashangaa ule usiku ambao alienda kanisani, kama alikuwa na nia njema. Je, mchungaji alitoa wito wa madhabahuni? Je, alikemea dhambi, na mtu huyo akawa na nafasi? Au alitoka kama mnyama? Je, huyo mtu, machoni pa Mungu, alikuwa mwana wa Mungu?

93 Wazieni mambo hayo, marafiki. Ni muhimu. Sio tu muhimu, ndilo jambo muhimu zaidi kwako saa hii. Huu ndio wakati ambao utatoa uamuzi wako. Huu ndio wakati ambapo unaweza

kufanya uamuzi wako wa maisha haya, kwa ajili ya maisha yajayo. Naomba uufanye wakati tukiomba.

94 Baba wa Mbinguni, tunaposoma katika Biblia juu ya yale uliyosema kuhusu dhambi, na wale wanaoitenda wala hawatubu. Tunatambua maana ya kufa bila kumjua Mungu. Tunajua hilo kwa uzoefu wa wengine, ambao tumewaona wakiondoka. Wale waliokusudia, wale walioliahirisha kwa muda mrefu kupita kiasi. Mungu, wale ambao wamekiri wala hawakumiliki yale waliyosema kuwa wanayo. Wale ambao walikuwa wametenda kama Wakristo, na hata hivyo hawakuwa Mkristo kamwe. Maisha yao yalilithibitisha hilo, nacho kifo chao kikalidhihirisha.

95 Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba utazungumza na kila moyo hapa usiku wa leo. Na mimi mwenyewe, Bwana, kwa kuwa mvivu, kwa mambo mengi ambayo ningeweza kufanya wala sikuyafanya, ninakiri makosa yangu. Ninakiri makosa ya watu hawa. Nakiri makosa ya taifa hili. Ninakuomba uturehemu, Bwana. Nina watoto watatu wadogo huko wa kulea. Nasi tunaishi hapa mahali penye joto, na, Mungu, hakuna haja ya kukimbia. Unajua yote kuyahusu. Mungu, nataka kuwa sawa na Wewe.

96 Siku moja, kama bomu la atomiki halitatupata, ajali ya barabarani itatupata. Ajali isipotupata, ugonjwa fulani utatupata. Kitu fulani hakina budi kutuchukua. Lakini tuna furaha sana kujua kwamba kuna njia ya kuepukia. "Jina la Bwana ni ngo—ngome, na wenye haki huikimbilia wakawa salama." Mungu, jalia rafiki mwenye dhambi, usiku wa leo, mvulana, msichana, mwanamume au mwanamke, auone mlango uliofunguliwa, fursa, na kumkimbilia Kristo saa hii.

97 Sasa wakati tumeinamisha vichwa vyetu, kuna wengine hapa, ama, najua kunao wengine hapa ambao wangependa kusema, kwa mkono ulioinuliwa kwa Mungu, "Ninayaonea aibu maisha yangu. Nami na—nataka kukiri makosa yangu mbele za Mungu, na kuomba rehema." Inua mkono wako kwa Mungu. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Kuna wengi wenu, wengi wenu. Naam. Kuna wengi wenu hapa, pia, ambao . . . Mungu akubariki.

98 Wengi wenu hapa, ambao mmekiri Ukristo kwa muda mrefu, nanyi mnajua kwamba mmeshindwa kufuata nyayo za Mungu, mnajua kwamba mnafanya mambo sasa hivi ambayo hampaswi kufanya. Na mnaenda, bila kuyakiri, mkielea tu ovyo ovyo kwa kufuata mkondo. Mkitazama vipindi ambavyo hampaswi kutazama. Mkiangalia magazeti na kusoma vitabu ambavyo hampaswi kusoma. Haifai kwa Wakristo. Mkisikiliza mizaha mi—michafu sana na kinyaa na masizi mnayojua hampaswi kusikiliza; wanaume kwa wanawake. Unajua mahali ambapo

ungaliweza kunena wala hukufanya hivyo, nawe una hatia, labda, dhambi ya kutotenda.

99 Sijui kama ungeinua mkono wako kwa Kristo, akurehemu, na kukusamehe. Inua mkono wako. Mungu akubariki, ewe msichana; wakati huyo mwanamke akitoka, kuja madhabahuni, kuungama yake. Inua mkono wako kwa Mungu. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli, bwana. Hiyo ni kweli. Mungu akubariki. Inua mkono wako. Unajua umefanya kosa.

100 Sijui kama una ujasiri, usiku wa leo, kukutana nami hapa madhabahuni. Hebu tupige magoti hapa na kusema, "Mungu, uturehemu sisi sote. Tunakuhitaji Wewe." Mungu akubariki, mama.

101 Kuwaona hawa wasichana wakija, wakilia, uzima mbele yao! Wako kwenye njia panda. Wao ni waathirika wa mazingira. Ati nini? Je, mnatambua, enyi wazee, tulipokuwa wavulana, wavulana wetu wana majaribio mara kumi ya yale tuliyokuwa nayo? Dada, je, unatambua kwamba binti yako ana majaribu mara kumi ya yale uliyokuwa nayo ulipokuwa msichana? Binti yake atakuwa na nini? Angalia hayo mambo, picha ambazo ibilisi anachora.

102 Loo, jinsi tunavyopaswa kuomba! Sasa tutawarudia tena. Ndugu, unatambua kwamba hatuombi nusu ya vile baba zetu walivyoomba? Mchungaji, unajua hatuweki muda mwingi magotini mwetu kama wachungaji waliotutangulia walivyofanya? Enyi wanawake, mnatambua kuwa humfundishi binti yako, na kuomba pamoja naye usiku, kama mama yako alivyokufanyia? Basi, vipi kuhusu hilo, ni nani aliye na hatia? Tuna hatia. Hakuna njia ya kulikwepa. Tuna hatia.

103 Nina hatia. Nina hatia ya kutofanya kazi ya Mungu, kama ninavyopaswa kufanya. Ninakiri, kwamba nina hatia. Ninamwomba Mungu anirehemu. Ninatazama hapa nje na kuona fursa ambazo nimekosa, kwa sababu ya vitu vidogo, vidogo, maskini mambo yasiyo na faida ambayo hayakuwa na maana yoyote. Ninajionea aibu, kama mhudumu wa Injili mbele zenu. Ninatubu mbele za Mungu, na kumwomba Mungu anisamehe, na kanisa linisamehe, kwa kuwa mvivu hivi kuhusu kazi ya Mungu. Kwa neema ya Mungu, na kwa msaada wa Mungu, si—sitasikiliza yale . . . Kila mtu akijaribu kukwambia la kufanya. Wana mpango. Wana jambo kwako kufanya. Upuuzi. Najua mpango wa Mungu; imeandikwa hapa katika Biblia. Nami ninajionea aibu kama mhudumu wa Injili. Watu milioni moja walioletwa; ninapaswa kuwa na watu milioni kumi walioletwa. Mimi niko nyuma sana.

104 Na wewe je? Ni watu wangapi ambao umeleta tangu umekuwa katika Kristo? Ukristo huenda tu kutoka kwa mmoja hadi mwingine. Umewaleta watu wangapi tangu uwe Mkristo? Ikiwa huleti watu, una hatia, wewe ni tasa, umeliletea aibu

Kanisa na Injili. Je, ni watu wangapi unaowaleta kwenye mkutano wa maombi wa Jumatano usiku? Ikiwa hufanyi hivyo, unapaswa kujionea aibu mbele za Kristo. Una hatia, na mahali pako ni madhabahuni. Ninakualika uje pamoja nami, kwa toba.

105 Ndipo mtainamisha vichwa vyenu, na kuendelea kuviinamisha kwa dakika moja, huku nikihisi hatia yangu na ningependa kutubu. Inamisha tu kichwa chako.

106 Baba yetu wa Mbinguni, ninainama juu ya madhabahu hii na kuomba msamaha wa dhambi yangu. Ninaomba msamaha wa dhambi za wale wanaoizunguka madhabahu. Ninaomba msamaha kwa ajili ya kanisa hili, kwa ajili ya mwili—kwa ajili ya kundi la waaminio nchini na kimataifa. Ninaomba rehema kwa ajili yetu, kwa kuwa wavivu hivi kuhusu mambo ya Ufalme. Ninaomba kwamba utusamehe dhambi zetu, na kuyaondoa makosa ye—ye—yetu. Na utusamehe kwa kuwa wapumbavu sana, kwa ajili ya upumbavu wa watu. Jinsi tulivyopungukiwa! Jinsi tumechukua mazoezi ya mwili! Jinsi tumefanya yale hatukupaswa kufanya! Jinsi tulivyotenda dhambi mbele Zako!

107 Na katika mkutano huu wa Jumapili usiku, Baba, tukimwona nabii wa Biblia mwenye haya, tunaona haya usiku wa leo. Ninaona haya mbele Zako, kwa sababu ya dhambi za watu. Watu, taifa langu, watu wangu, nimewaonea aibu, Bwana. Kuona wasichana wetu wakitembea mitaani na kutenda jinsi wanavyotenda! Kuona ukahaba, vijana wanaume wakiishi katika—katika namna zote za maisha! Kuwaona wakikaa nyumbani bila kwenda kanisani, na kusoma maskini magazeti wasiopaswa kusoma! Wakiangalia vipindi visivyokaguliwa! Wakisikiliza mizaha michafu ya Hollywood! Wakisikiliza muziki wa kale wa bugi-wugi wa ibilisi, ambao umeanguliwa kutoka kwa watu wenye sifa mbaya na wenye dhamiri chafu sana, ushawishi wa ibilisi, ili kuvuvia mwendeleo wa kazi za ibilisi!

108 Ee Mungu, ninajionea aibu kwa kutokukemea jinsi inipasavyo. Ee Mungu, niondolee hatia yangu. Ninakuomba ufanye hivyo. Ninakuomba uwasamehe watu hawa walio hapa, kwanza, sisi sote. Tusaidie tuinuke kutoka kwenye madhabahu hii kama wanaume na wanawake wapya. Tusaidie tutoke hapa kama iwapasavyo Wakristo kwenda.

109 Tusaidie "Kuweka kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi, ili tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu." Tukiangalia si televisheni, sio kuwaangalia wachekeshaji wa ulimwengu, bali, "Tukimtazama Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu, Bwana Yesu Kristo, Yeye aliyeidharau aibu ya msalaba na kuichukua kwa ajili yetu, na kuteswa nje ya lango, ili awatakase watu kwa Damu Yake."

110 Utusafishe na uovu wote, na utuchukue kama watoto Wako mwenyewe, usiku wa leo, na utupokee katika maombi haya ya toba. Na utupe, Bwana, amani na furaha. Na jalia vitanda vyote, usiku wa leo, tukiwa tumelala, tukitafakari juu ya mkutano wa usiku huu, na tutafakari hali za ulimwengu, ambazo Biblia imetufunulia sasa. Tujalie, tunapoliwazia, huku nyuso zetu zimetokeza kwa aibu, na naomba ulete amani na furaha kwa kila moyo. Tunatubu, Bwana, mbele Zako, kwenye madhababu hii.

111 Mungu, nisaidie ninapojitokeza sasa, kwa imani, na kuomba ya kwamba liko katika mapenzi Yako, ya kwamba mamia mengi, mengi, mengi ya watu waweze kuletwa Kwako. Na unisaidie kuwa na imani na ujasiri, ninapoendelea mbele; pasipo kumtazamia mtu yeyote ila Wewe, Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu. Mungu, tujalie.

112 Msamehe kila shemasi wa kanisa hili. Msamehe mchungaji. Wasamehe washiriki walei, Bwana. Msamehe kila mtu, dhambi zetu zote. Utusamehe, Bwana. Msamehe kila mgeni langoni petu. Na jalia tuhisi nguvu za Roho Mtakatifu maishani mwetu, kwa sababu sisi ni wanyenyekevu mbele Zako, usiku wa leo, tukitubu kwa moyo wetu wote, kwamba utatupokea na kutufanya kuwa watu wanyenyekevu, watulivu, waliotakaswa na wanyenyekevu kwa ajili ya huduma Yako. Tujalie baraka hii, Bwana, kwenye madhababu tuliyo juu yake. Lijalie. Na tuinamishe kichwa chetu na mioyo yetu mbele Zako. Katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu, tunaomba haya. Amina, na amina.

> Mimi ni wako, Bwana, nimeisikia Sauti Yako,
> Na ikaniambia upendo Wako;
> Jinsi ninavyotamani kuinuka katika mikono
> ya imani,
> Na nivutwe karibu zaidi na Wewe.
>
> Univute karibu, karibu zaidi, Bwana
> mbarikiwa,
> Msalabani pale ulipofia;
> Univute karibu, karibu zaidi, Bwana
> mbarikiwa,
> Ubavuni Mwako wa thamani, unaovuja damu.

113 Kando ya madhababu, usiku wa leo, miongoni mwa ndugu zangu walio hapa madhababuni, ninafurahi kuona, usiku wa leo, wanaume wengi kama walivyo wanawake. Kwa kawaida, ni wanawake ambao wanaweza kuvunjika kwa urahisi. Mioyo yao, kuna kitu fulani kuwahusu, kinachoweza kuguswa kwa urahisi kwa sababu ya kike. Nao—nao ni wanawake, na wakati mwingine unaweza kuwagusa. Lakini nina furaha sana kuona Roho Mtakatifu anaweza kuwagusa wanaume, pia, na kuwaleta madhababuni.

114 Na sijui ni wangapi wenu madhababuni, ambao wamepiga magoti sasa, ambao wanahisi kwamba umejiweka wakfu kwa

Mungu, kwamba unatoka hapa usiku wa leo, kuishi maisha bora zaidi, kwa neema ya Mungu, na kufanya mengi zaidi kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, na kwa ajili Yake. Naomba uinue mkono wako kwa Kristo, kama uko karibu na madhabahu, useme, "Ninaamini kwamba sasa nimetubu." Mungu akubariki.

115 Ni wangapi wenu huko nyuma mnaojisikia kwamba mlitubu kitini mwenu; unajisikia kwamba unataka kufanya vizuri zaidi? Mungu akubariki.

Sasa hebu na tusimame.

116 Ninyi hapa madhabahuni, geukeni *hivi*, tafadhali. Sasa, ninyi hapa madhabahuni, inueni mikono yenu huko nje, ya kwamba mnatamani maombi yao, mpate kuendelea mbele. Je, mtainua mikono yenu kwa wale walio kwenye kusanyiko? Vema. Sasa inueni mikono yenu hapa nyuma, madhabahuni hapa, kwamba huenda mkatamani maombi yao, pia. Hata tutaweza . . . Mungu atatusaidia kufanya hivyo. Bwana Yesu na atubariki.

Sasa, msisahau ibada ya Jumapili usiku.

117 Una neno la kusema, Ndugu Neville? [Ndugu Neville anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Jumanne na Jumatano usiku . . . Misheni hiyo iko wapi? [Ndugu Neville anajibu.] Soko la Magharibi 1628, Jumanne hii ijayo na Jumatano usiku.

118 Na kisha Jumamosi na Jumapili, nitakuwa Madisonville, Kentucky, kwenye jumba la mikutano kule. Na kisha tuendelee hadi New York.

119 Sasa, sababu ya sisi kuondoka mapema, nina mama mkwe ambaye ni mgonjwa sana, sana, na wananiita. Sasa hebu . . .

120 Una neno la kusema, Ndugu Neville? [Ndugu Neville anasema, "La."—Mh.] Hakuna.

121 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo, tunapoomba. Vema. Polepole sasa:

> Mungu awe nanyi hata tutapokutana tena!
> Kwa . . .

56-1125E Nabii Mwenye Haya
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org